## 4.0 KISWAHILI

Uchanganuzi wa matokeo ya mwaka wa 2011 umefanywa kwa kulinganishwa na yale ya miaka ifuatayo: 2008 ,2009. na 2010

***Jedwali 8: Matokeo ya KCPE Kiswahili ya 2008 hadi 2011***

| | **2008** | | **2009** | | **2010** | | **2011** | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Lugha** | **Insha** | **Lugha** | **Insha** | **Lugha** | **Insha** | **Lugha** | **Insha** |
| | **50** | **40** | **50** | **40** | **50** | **40** | **50** | **40** |
| **Alama ya wastani** | 28.30 | 18.40 | 28.65 | 21.48 | 26.38 | 20.12 | **20.77** | **21.89** |
| **Alama iliyotuzwa watahiniwa wengi** | 30 | 18 | 30 | 20 | 27 | 20 | 20 | 20 |
| **Alama ya juu iliyotuzwa** | 50 | 40 | 50 | 40 | 49 | 39 | 47 | 40 |

Jedwali hili linaonyesha kwamba:

**Katika lugha**:

a) Alama ya wastani ilishuka kutoka **26.38** mwaka wa 2010 hadi **20.77** mwaka wa 2011.

b) Alama ya juu iliyoweza kutuzwa mwaka wa 2011 ni **47** tofauti na **49** ya mwaka wa 2010.

c) Alama iliyotuzwa watahiniwa wengi ni **20** tofauti na **27** ya 2010.

d) Alama ya wastani katika karatasi hii inaendelea kushuka.

**Katika Insha:**

a) Alama ya wastani ilipanda kutoka **20.12** ya mwaka wa 2010 hadi **21.88** mwaka wa 2011.


b) Alama ya juu zaidi iliyoweza kutuzwa mwaka wa 2011 ni **40** tofauti na **39** ya mwaka wa 2010.

c) Alama iliyotuzwa watahiniwa wengi ni **20.**

d) Ingawa alama wastani inaelekea kufikia kiwango kinachokubaliwa, alama hii bado haijawa thabiti, inayumba mwaka baada ya mwaka.

Mchoro ufuatao unaonyesha jinsi alama za sehemu za lugha na insha zilivyojitawanya.

**Mchoro wa tatu**





## 4.1 SEHEMU YA KWANZA: LUGHA

### 4.1.1 Uchanganuzi wa Maswali Maalum

Mchoro ufuatao unaonyesha asilimia ya watahiniwa ambao walipata jibu sahihi katika kila swali.

**Mchoro wa nne**




### 4.1.2 Uchanganuzi wa maswali yaliyowatatiza watahiniwa.

Katika mwaka wa 2011, yapo maswali ambayo yalionekana kuwatatiza watahiniwa. Watahiniwa waliopata majibu sahihi kwa maswali haya walikuwa chini ya asilimia thelathini (30%). Maswali yafuatayo ndiyo yanayochukuliwa kuwa yaliwatatiza watahiniwa zaidi: Swali 1, 2, 18, 20, 26, 33, 36, 38, 39 , 40 na 43.

***Jedwali 9: Maswali ambayo yaliwatatiza watahiniwa***

| Maswali | 1 | 2 | 18 | 20 | 26 | 33 | 36 | 38 | 39 | 40 | 43 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Asilimia ya watahiniwa waliopata jibu sahihi | 10.35 | 24.14 | 25.45 | 28.26 | 23.03 | 17.50 | 18.74 | 12.24 | 5.35 | 20.18 | 23.46 |
| Asilimia ya wastani ya mswali yale mengine | 26.03 | 22.33 | 22.48 | 21.73 | 22.80 | 22.42 | 22.96 | 20.88 | 21.88 | 20.21 | 22.21 |

### 4.1.3 Ruwaza za Majibu

**Maswali 1 mpaka 15.**

*Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.*

Wakazi wa vitongoji duni __1__ na matatizo mengi. Asilimia kubwa ya waja hapa __2__ __3__ aila __4__, katika mitaa ya mabwanyenye __5__ na vitongoji hivi, hali ni tofauti; majumba yenye kuvutia yamepamba mazingira humo. Maisha ya makundi haya mawili __6__. Wana wa matajiri hupata mahitaji __7__ huku maskini __8__ kwa ukosefu. Ama kwa kweli __9__.

**Swali la 1**

A. wametwaliwa B. wamekabidhiwa C. wametengwa D. wametingwa

**Matokeo ya swali la 1**

| Majibu | A | B | C | *D |
|---|---|---|---|---|
| **Asilimia ya watahiniwa waliochagua jibu hili** | 8.98 | 67.85 | 12.16 | 10.35 |
| **Alama yao ya wastani ya maswali yale mengine** | 21,12 | 20.45 | 17.74 | 26.03 |

Swali hili lilitahini matumizi ya msamiati mwafaka kulingana na maneno yaliyo katika ujirani wa neno lililotahiniwa. Mtahiniwa alihitajika kuchunguza neno" **matatizo** na kulihusisha na mojawapo ya viteuliwa vilivyotolewa ili kupata jibu sahihi. Watahiniwa wengi walikimbilia neno,'**wamekabidhiwa**', wakidhani ni,'**wamekabiliwa,**' ambalo ndilo kisawe cha neno ,'**wametingwa**', ambalo ndilo jibu la swali hili.

**Swali la 2**

A. haiwezi B. hawawezi C. haziwezi D. hamuwezi

**Matokeo ya swali la 2**

| Majibu | *A | B | C* | D |
|---|---|---|---|---|
| **Asilimia ya watahiniwa waliochagua jibu hili** | 24.14 | 69.15 | 4.75 | 1.29 |
| **Alama yao ya wastani ya maswali yale mengine** | 22.33 | 20.46 | 18.84 | 18.80 |

Swali hili lilitahini viambishi ngeli na upatansho wa kisarufi. Ruwaza za majibu zinaonyesha kwamba wanafunzi wengi, ama wana changamoto katika mada hii, au hawasomi maswali ipasavyo kabla ya kuteua jibu. Watahiniwa wengi walichagua jibu **B: hawawezi** bila kuzingatia kwamba walihitajika kuzungumzia nomino, **aslimia** wala si **waja.** Kipatanishi cha **asilimia** ni **-i-** kinyume na **–wa-** ambacho ni kipatanishi cha **waja.**

**Swali la 18**

Chagua neno ambalo limetumia silabi changamano.

A. Mbuga
B. Kituta
C. Ziwa
D. Utulivu

**Matokeo ya swali la 18**

| Majibu | A* | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| **Asilimia ya watahiniwa waliochagua jibu hili** | 25.45 | 23.76 | 14.65 | 35.26 |
| **Alama yao ya wastani ya maswali yale mengine** | 22.48 | 20.36 | 19.06 | 20.51 |

Swali hili lilitahini stadi ya matamshi bora, hususan aina za silabi. Mtahihiniwa alihitajika kutofautisha kati ya silabi ambazo ni ngumu kutamka (changamano), kwani zinaundwa kwa sauti mbili ambazo sharti zitamkwe pamoja. Ingawa asilimia inayoonyesha ugumu wa swali inakubalika (25.45), imebainika kwamba wanafunzi wengi walishindwa kuelewa maana ya neno changamano, jambo ambalo laonyesha kutofunzwa kwa istilahi hii ambayo inapatikana katika silabasi ya darasa la pili. Hata hivyo wanafunzi waliopata jibu sahihi ndio walio na alama ya wastani ya juu katika maswali yale mengine.

**Swali la 20**

Chagua sentensi yenye vivumishi

A. Mwashi amejenga nyumba juu ya mlima.
B. Yule aliimba vizuri mno akatuzwa.
C. Nokoa atafika hapa hivi punde.
D. Wanafunzi wengi walifaulu mtihani huo

**Matokeo ya swali la 20**

| Majibu | A | B | C | D* |
|---|---|---|---|---|
| **Asilimia ya watahiniwa waliochagua jibu hili** | 17.81 | 38.73 | 14.43 | 28.26 |
| **Alama yao ya wastani ya maswali yale mengine** | 19.29 | 21.00 | 20.05 | 21.73 |

Swali hili lilitahini uwezo wa mtahiniwa wa kutumia ujuzi wake wa aina za maneno. Asilimia kubwa ya watahiniwa ilichagua jibu, **B.** Hili linadhihirisha kwamba wengi bado hawajatofautisha kati ya vivumishi na vielezi. Hata hivyo, kiwango cha ugumu wa swali hili (28.26) kinakubalika. Isitoshe, watahiniwa waliopata jibu sahihi ndio walio na alama ya wastani ya juu katika maswali yale mengine.

**Swali la 26**

Ni sentensi ipi sahihi?

A. Hewalla!Nitakusaidia.
B. Kefule! Naomba maji.
C. Oyee! Tumeshindwa.
D. Hamadi!Amekuja.

**Matokeo ya swali la 26**

| **Majibu** | A* | **B** | C | D |
|---|---|---|---|---|
| **Asilimia ya watahiniwa waliochagua jibu hili** | 23.03 | 14.48 | 43.21 | 18.47 |
| **Alama yao ya wastani ya maswali yale mengine** | 22.80 | 20.52 | 19.57 | 21.19 |

Swali hili lilitahini matumizi mwafaka ya vihisishi. Watahiniwa wengi walichagua jibu **C.** Inakisiwa kwamba hili lilitokana na athari za 'Sheng' ambapo neno **Oyee** linahusishwa na kutoridhika au kutofanikiwa.Wengine huenda hawakusoma neno la mwisho vyema. **Oyee** huenda na ushindi wala si ushinde.

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 – 40.*

Mfumo wa elimu nchini unatilia mkazo mafunzo mengine ambayo, japo yamo nje ya masomo ya kawaida, yanahusiana na kwenda sambamba na masomo hayo ya kawaida. Vyama vya wanafunzi shuleni vinachangia pakubwa kupitisha mafunzo hayo ya ziada

Vyama vya wanafunzi hutofautiana kulingana na majukumu. Mathalani, vipo vyama vya kidini, vya kitaaluma na vya michezo. Pia, kuna vyama vya kijamii kama vile Chama cha Kupambana na Matumizi Mabaya ya Dawa na vya kiuchumi kama vile Chama cha Wakulima Chipukizi.

Imedhihirika kwamba vyama vya wanafunzi vina **manufaa ya kuhusudiwa**. Hii ndiyo sababu shuleni, kila mwanafunzi anahimizwa kujiunga na angaa vyama viwili. Vyama vya wanafunzi huwasaidia kukuza vipawa na kuimarisha stadi za kujieleza. Haya hufikiwa kupitia kwa shughuli za vyama kama vile ukariri wa mashairi, mijadala, utegaji na uteguaji vitendawili, chemsha bongo na ulumbi. Aidha, vyama hivi huhimiza utangamano miongoni mwa wanachama kwani wao hujiona kuwa watu wenye mwelekeo mmoja. Vilevile utangamano wa kitaifa na kimataifa hujengeka.

Mwanafunzi ambaye amejiunga na vyama vya wanafunzi huweza kukabiliana na changamoto za maisha kwa urahisi kuliko yule ambaye hajawahi kujiunga na chama chochote. Katika vyama hivi, wanafunzi hufunzana mikakati na maarifa ya kutatua matatizo na mbinu za kuepuka mitego ya ujana. Kupitia kwa ushauri wa marika kwa mfano, mwanafunzi hushauriwa kuhusu masuala kama vile uteuzi wa marafiki, kuratibu muda, kujikubali na kuwakubali wenzake.

Hali kadhalika, mwanafunzi hujifunza maadili ya kijamii na kidini. Kupitia kwa vyama vya kidini na vinginevyo, yeye hujifunza kujistahi na kuwa na stahamala ya kidini, kiitikadi na kikabila. Kadhalika, majukumu ambayo mwanafunzi huenda akapewa hupalilia uwajibikaji, uaminifu na kipawa cha uongozi. Hata anapohitimu masomo yake, mwanafunzi huyu huendeleza sifa hizi.

Vijana wana nafasi kubwa katika kukabiliana na maovu ya kijamii kwani wao ndio wengi zaidi. Kupitia kwa vyama hivi, wanafunzi wanaweza kuwahamasisha wenzao dhidi ya tabia hasi kama vile kushiriki mapenzi kiholela, ulanguzi wa dawa za kulevya na kujiingiza katika burudani zisizofaa. Pia, shughuli na miradi ya vyama hivi huwawezesha wanafunzi kutumia nishati zao kwa njia ya kujinufaisha na kuepuka maovu. Kwa mfano, wanaweza kwenda kukwea milima, kufanya matembezi ya kukusanya pesa za kuwafadhili wahitaji, kuendeleza shughuli za kunadhifisha mazingira na kutembelea vituo vya mayatima na wazee.

Kushiriki katika vyama vya michezo hakumwezeshi mwanafunzi kuimarisha afya na kujenga misuli tu, bali pia huweza kuwa msingi wa kupata chanzo cha riziki baadaye. Wapo wachezaji maarufu ambao walitambua na kuviendeleza vipawa vyao kupitia kwa vyama vya aina hii, na hivi sasa wana uwezo wa kuyaendesha maisha yao na ya familia zao.

Ifahamike kuwa vyama vya wanafunzi vinapaswa kuwa msingi wa mshikamano na maridhiano. Visitumiwe kama vyombo vya kuwagawa wanafunzi kitabaka. Mwanafunzi hana budi kusawazisha muda anaotumia. Atenge muda wa shughuli za vyama na wa kudurusu masomo yake.

**Swali la 33**

Chagua jibu **lisilo sahihi** kwa mjibu wa taarifa.

A. Vyama vya wanafunzi huchangia kukuza ubunifu wa wanafunzi.
B. Vyama vyua wanafunzi huchangia kukuza uzalendo wa kimataifa.
C. Vyama vya wanafunzi huwasaidia kuimarisha uzalendo na mahusiano mema.
D. Vyama vya wanafunzi huwasaidia kuimarisha uhusiano na nchi nyingine.

**Matokeo ya swali la 33**

| **Majibu** | A | B* | C | D |
|---|---|---|---|---|
| **Asilimia ya watahiniwa waliochagua jibu hili** | 23.09 | 17.50 | 12.41 | 46.10 |
| **Alama yao ya wastani ya maswali yale mengine** | 20.03 | 22.42 | 18.60 | 21.09 |

Mtahiniwa alihitajika kuchagua jibu **lisilo sahihi** kulingana na kifungu. Hata hivyo, wengi walipuuza kiini cha swali na kuchagua jibu ambalo kwa kweli ni sahihi kulingana na kifungu. Maelekezo ya swali ni muhimu kusisitizwa na walimu.

**Swali la 36**

Kulingana na kifungu, vijana wanaweza kudhihirisha uwajibikaji katika jamii kupitia:

A. Kuwapinga walanguzi wa dawa za kulevya na kuepuka burudani.
B. Kufanya matembezi anuwai ya kukusanya pesa.
C. Kushiriki katika miradi ya kuwaauni wanyonge.
D. Kuendeleza shughuli za kuhifadhi mazingia na kutembea milimani.

**Matokeo ya swali la 36**

| **Majibu** | A | B | C* | D |
|---|---|---|---|---|
| **Asilimia ya watahiniwa waliochagua jibu hili** | 48.46 | 10.28 | 18.74 | 21.69 |
| **Alama yao ya wastani ya maswali yale mengine** | 20.68 | 18.93 | 22.96 | 19.92 |

Swali hili lilitahini stadi ya matumizi. Mtahiniwa alihitajika kutumia ufahamu wake wa yaliyomo katika kifungu kujibu swali. Hata hivyo, asilimia kubwa ya watahiniwa ilichagua jibu **A.** Pengine **hawa** walivutiwa zaidi na matumizi ya kirai,**'walanguzi wa dawa za kulevya**. Ni muhimu walimu kuwazoesha wanafunzi wao kujibu aina hii ya maswali. Kutokana na jedwali hili ni dhahiri kwamba, japo watahiniwa wengi walikosa jibu sahihi, alama ya wastani ya waliopata jibu sahihi katika maswali mengine ilikuwa juu kidogo kuliko ya wale waliokosa jibu hilo.

**Swali la 39**

Maoni ya mwandishi katika aya ya mwisho ni kwamba:

A. Vyama vya wanafunzi vinaweza kuvuruga usawa katika jamii.
B. Vyama vya wanafunzi ndio msingi wa kumsaidia mwanafunzi kutumia muda wake darasani.
C. Vyama vya wanafunzi vinaweza kuvuruga masomo katika darasa.
D. Vyama vya wanafunzi ndio msingi wa kuimarisha umoja na maelewano katika jamii.

**Matokeo ya swali la 39**

| Majibu | A* | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| Asilimia ya watahiniwa waliochagua jibu hili | 5.35 | 31.41 | 12.91 | 49.55 |
| Alama yao ya wastani ya maswali yale mengine | 21.88 | 19.44 | 20.94 | 21.43 |

Swali hili lilipima stadi ya kutathmini. Watahiniwa wengi walivutiwa na kirai,'**umoja na maelewano'**, na kuteua jibu **D** japo jibu sahihi lilikuwa **A.** Ni muhimu walimu kuwasisitizia wanafunzi umuhimu wa kusoma viteuliwa vyema na kuvihusisha na yaliyomo kabla ya kuteua. Maswali ya ufahamu yanayopima stadi hii yaangaziwe zaidi.

**Swali la 40**

Kulingana na kifungu, **manufaa ya kuhusudiwa** ni:

A. manufaa yanayowafaidi wengi
B. manufaa yanayowavutia wengi
C. manufaa yasiyosahaulika kwa urahisi
D. manufaa yasiyopatikana kwa urahisi.

**Matokeo ya swali la 40**

| Majibu | A | B* | C* | D |
|---|---|---|---|---|
| Asilimia ya watahiniwa waliochagua jibu hili | 63.35 | 20.18 | 8.81 | 6.89 |
| Alama yao ya wastani ya maswali yale mengine | 21.54 | 20.21 | 18.29 | 18.45 |

Asilimia kubwa ya watahiniwa ilichagua jibu **A** kwa kutoelewa maana ya **kuhusudiwa.** Kitu kinachowavutia wengi si lazima kiwe na faida kwa wengi. Watahiniwa hawakusoma taarifa vyema.

**Swali la 43**

Mazingira ya kuvutia yalimwathiri Msimulizi kwani:

A. Aliduwaa na kujisahau.
B. Alifurahia upepo na kujisahau.
C. Alizubaa na kupuuza sheria za usafiri.
D. Alipumbaaa na kupinga sheria za usafiri.

**Matokeo ya swali la 43**

| Majibu | A | B | C* | D |
|---|---|---|---|---|
| Asilimia ya watahiniwa waliochagua jibu hili | 30.55 | 31.20 | 23.46 | 13.70 |
| Alama yao ya wastani ya maswali yale mengine | 21.21 | 19.65 | 22.21 | 19.91 |

Watahiniwa wengi walivutiwa na jibu **B.** Walishindwa kutumia ujuzi wao wa yaliyomo katika kifungu kujibu swali. Msimulizi hakujisahau.alikosa tu kufunga mkanda wa usalama.

## 4.2 SEHEMU YA PILI – INSHA

Katika mwaka wa **2011** swali lilikuwa:-

Andika insha isiyopungua ukurasa mmoja na nusu ukifuata maagizo uliyopewa.

**Mwandikie barua rafiki yako ukimshauri kuhusu jinsi ya kujiandaa vyema kwa mtihani wa KCPE.**

Swali hili lilitahini uandishi wa tungo amilifu, hususan barua ya kirafiki/barua ya kidugu. Mtahiniwa alihitajika kumwandikia barua rafiki yake akimpa ushauri kuhusu namna ya kujitayarishia mtihani wake.Yafuatayo yalihitajika kuzingatiwa:

**a) Maudhui/yaliyomo**

Hapa mtahiniwa alihitajika kujadili masuala yanayohusiana na maandalizi kwa mtihani. Baadhi ya hoja ambazo zilitarajiwa ni:

i) Kudurusu kila somo kwa kina
ii) Kufanya mazoezi katika masomo yote
iii) Kujiunga na vikundi vya kujadiliana masuala tata
iv) Kufanya majaribio kupitiakwa mitihani ya awali
v) Kuwaomba walimu kumfafanulia mada ambazo hakuzikuelewa.
vi) Kujiamini
vii) Kuepuka wasiwasi
viii) Kudumisha nidhamu
ix) Kufanya mazoezi ya mwili. ili kuimarisha misuli na kunoa ubongo zaidi
x) Kula vyema/lishe bora
xi) Kupumzika

**b) Muundo na Mtindo**

Muundo/sura ya barua ya kirafiki ilihitajika kuzingatiwa, yaani:

i) Anwani ya mwandishi
ii) Mtajo
iii) Mpangilio wa kazi ki-aya
iv) Kimalizio
v) Mtindo wa uwasilishaji uwe wa barua.

### 4.2.1 Vigeso vya usahihishaji

Yafuatayo ni maelezo yanayoonyesha jinsi watahiniwa wanavyotengwa katika viwango/vitengo vinne maalum, na mambo ambayo yananzingatiwa ili kumtuza mtahiniwa kiasi fulani cha alama katika vitengo hivi vinne. Vifuatavyo ndivyo vitengo (makundi) vya alama:

(i) 01 – 10
(ii) 11 – 20
(iii) 21 – 30
(iv) 31 – 40

### 4.2.2 Kundi la kwanza (alama 01 – 10)

Watahiniwa katika kiwango hiki hawamudu kujieleza katika Kiswahili. Watahiniwa wanaopata alama 01-05 hasa huwa na mtindo hafifu sana wa kujieleza. Insha zao hukosa muumano wa mawazo. Baadhi hujieleza kwa kuchanganya maneno ya Kiswahili, Kiingereza na hata lugha zao za mama. Wengine hutumia maneno yasiyoeleweka kabisa. Msamiati hutumiwa kiholela bila uwiano wowote. Sheria za uakifishaji hupunzwa kabisa. Udhaifu wao kimawasiliano huwakosesha kuikuza mada/maudhui ya swali walilopewa.

Watahiniwa wanaotuzwa alama 06-10 hudiriki kujieleza kwa Kiswahili, japo kwa mtindo hafifu. Hata hivyo, insha zao huwa na makosa mengi ya sarufi na hijai ambayo huufifilisha usimulizi/kujileza kwao. Hawa pia huwa wamepotoka kimaudhui/upande na wengi huhamisha sheria za lugha zao za mama hadi Kiswahili( huwa na athari nyingi za lugha ya mama).

**Mtungo wa kwanza**

Umepewa dakika 40 kuandika insha yako.

Andika insha isiyopungua ukurasa mmoja na nusu ukifuata maagizo uliyopewa.

Mwandikie rafiki yako barua ukimshauri kuhusu namna ya kujiandaa vyema kwa mtihani wa KCPE.

[illegible]

[illegible]

Mtahiniwa huyu ameshindwa kabisa kuwasiliana. Maneno anayotumia hayaeleweki, wala hayajulikani ni ya lugha gani. Kazi yake imekosa uakifishaji ufaao, na hati yake ni mbaya na hajapanga mawazo ki-aya. Mtahiniwa wa aina hii kwa kawaida hupata bakshishi tu.

Alama iliyotuzwa: **01**

**Mtungo wa Pili**

**Umepewa dakika 40 kuandika insha yako.**

Andika insha isiyopungua ukurasa mmoja na nusu ukifuata maagizo uliyopewa.

Mwandikie rafiki yako barua ukimshauri kuhusu namna ya kujiandaa vyema kwa mtihani wa KCPE.

MSINGI YA,
KUKUNOI,
53 LONGISA.
13-11-2011.

KWA RAFIKI KIRUI.

Hujambo rafiki yangu kirui natumai yuko msima kama kiag'onga mukiendelea na mtihani wenu wa K.C.P.E. Nami niko msima.

Ujumbe kwangu kukuandikia hiki barua ni kuambau kukujulisha kwamba tunaendelea na mtihani wetu wa K.C.P.E. Ukweli nikuambia tulianza mtihani wetu jusi tu tarehe nane, mwezi wa kumi na moja, mwaka wa elfa mbili na kumi na mbili.

Karatasi ya kuansa kufika mbele yetu. yenyetulikuwa tumengoja kwa hamu na kamu, ilikuwa ni karatasi ya hesabati. Tulipobatiwa karatasi kidoko ya kuandikia jina, na shule yetu. tulianza mtihani wetu wakwanzu iliyo ya ijukua muda wa masaa mawili na dakika kumi na tano saa mbili na nusa ya hasubuhi. na tuka weka kikomo saa inne na dakika arobaini na tano.

Tulitoka nje huku mwalimu wetu akituambia "muende nje kwa dakika ishirini." Tulirundi ndani huku tumejawa nafuraha tale ya kuandoa uoka. karadasi ingine ya kingeresa ikaletwa. tulimalisa hiyo huku tukienda kuhuka saa sita na arbaini karatasi ilijukua muda wa masaa mawili na arobaini

Tulipo toka kishuka kiongele ilkalia kengeresa (composition) tukapatiwa, iliyajukua muda wa dakika arobaini.

Basi sasa tunaendebea vizuri katika masomo yetu huku tukitarajia matokeo bora.

kweheri salamia baba, mama, mandugu zangu, dada zangu, yanya na babu huwambie mimi sita kuja nyumba kwanza tukimalisa mtihani nita pitia kwa rafiki yangu mwingine tusalimiane na yeye alafu kwa siku ingine nita kuwa yumbani k

Kutoka rafiki
yako mbendwa
KIPTONO BETT.

Insha hii ina makosa mengi mno ya sarufi na hijai. Uakifishaji wake ni mbaya mno. Japo ana ufahamu kiasi wa suala analoandikia kujieleza kwake kumepungukiwa mno. Anahadithia aliyofanya badala ya kutoa ushauri.Insha imejaaa makosa ya hijai ambayo yanatokana na athari za lugha ya mama.Kwa mfano:

i) 'Msima' badala ya 'mzima'
ii) 'Tulirundi' badala ya 'tulirudi'
iii) 'Kamu' badala ya 'ghamu'

Hata hivyo mtahiniwa ametumia mtindo na muundo wa barua. Ametumia lugha ya Kiswahili ijapo mtungo wake umeumepokwa mvuto na makosa mengi ya safuri na hijai.

Alama iliyotuzwa: **04**

### 4.2.3 Kundi la Pili (alama 11 – 20)

Kundi hili huwa na watahiniwa ambao wanaimudu lugha kiasi. Wanaweza kujieleza/kusimulia kwa sentensi/kauli zinazoleta maana. Wale wanaotuzwa alama 11-14 huwa na makosa mengi ya sarufi na hijai na insha zao hukosa mtiririko mzuri wa mawazo.Wengi huwa bado na athari za lugha za kwanza/lugha za mama.

Wanaotuzwa alama 16-20 huwa wameimudu mada kiasi na mtindo wao wa uwasilishaji huwa bora zaidi, ingawa bado huwa chini ya wastani. Wanaweza kutumia msamiati wa kuvutia hapa na pale japo kwa kawaida wengi huutumia msamiati wenyewe vibaya. Insha zao kwa kawaida hutosheleza urefu.

**Mtungo wa Tatu**

**Umepewa dakika 40 kuandika insha yako.**

Andika insha isiyopungua ukurasa mmoja na nusu ukifuata maagizo uliyopewa.

Mwandikie rafiki yako barua ukimshauri kuhusu namna ya kujiandaa vyema kwa mtihani wa KCPE.

Shule ya msingi ya Lukesi
S. L. P 2222
Kitale
9-11-20011

Kwa rafiki mpendwa Juma

Nachukuwa fursa hii kukuandikia barua hii kwani ni mdamrefu hatuja onana ana kwa ana. Ni kidhani huko uliko usalama na buheri wa afya. Sisi huku nyumbani tu wazima bija, tu buheri wa afya. Ni kidhani pia huku shuleni uliko masomo yana kupeleka vyema. Napia hukuniliko maisha ya shale yana nipeleka vyema ni kisubiri kuukalia mtihani wangu wa kitaifa wa KCPE.

Nachukuwa wathija huu kukueleza umuhimu wa kujiandaa kwa mtihani wa KCPE unao kuja hivi karibuni mweze wa kumi na moja mwaka kesho. Najahamu kwamba huko shuleni umejiandaa vyema kwajili ya mtihani huo wa kitaifa. Unapaswa kujahamu kwamba, mkono mtupu hauramba na mtaka chavanguni shanti ainame.

Hundiyo wakati unapaswa kuwa kampu na vitabu bia uwe ukiwauliza walimu maswali kilasiku. Jambolingine ambalo unapaswa kujaham ni kwamba uepuke marafingi wale ambao hamana msingi namsimamo. Unapaswa kutafuta aina

tofauti gavilabu.

Lengo langa kuu kukuandikiya barua hini kukujuza umuhimu wakujiandaa kwa mtihani huwa KCPE. Jambo lakwanza ujange mazoezi yakutosha ambayo yata kuwezesha kula mbuka mambo uliyo ijasoma wakati utakuwa kwenye mtihani. Kabia usisome tu Somo ambalo unalipena peke yake, hiyo itakacha ngia kuchoka mapema sana. Ukumbuke haupaswi kusoma kupita hiasi kwani wingi wa jambo ni sumu.

Jambo lapili ni kwamba unaja udurusu vitabu vyachini kwani mtihani huo hautatoka katika Darasa lanane peke yake. Hayo yote ambayo ninakuelezea, mimi huwa naya jangamani meona gameni sendiya katika mitihani mingine. Unapo kuwa ukisoma uweuhimweka molambele kwani mdahamsahau njawake. Najahamu nivigumu kuamuka asubui na mabema kwajili yakusoma, likini unapaswa kujua mchamia juani hulia kivulini na mwegemea mpini hajinyoa.

Sina mengi yakausema bali nakusi ugazingatie yale ambayo nimekueleza nautaona mtihani unakuwa mwepesi. Kwahayo yote nakutakia kilalaheri katika mtihani wako na Mola akudariki

Mimi rafiki yako mpendwa

Wasilwa W Boaz.

Mtahiniwa huyu anaonyesha kuielewa mada. Hata hivyo imejaa makosa ya sarufi na hijai ambayo yanaufanya mtindo wake wa kujieleza kuwa hafifu mno.Mtahiniwa ana athari za lugha ya mama..Kwa mfano anatumia neno**: bia** badala ya **pia**. Kadhalika ,ana makosa ya kitahajia kama vile kuunganisha na kutenganisha maneno ambayo hayapaswi kuunganishwa/kutenganishwa.Tazama mifano:

i) 'Kilalaheri' badala ya 'kila la heri'
ii) 'Mudamrefu' badala ya 'muda mrefu'
iii) 'Usalama' badala ya 'u salama'
iv) 'Nam simamo' badala ya na 'msimamo'
v) 'Una paswa' badala ya 'unapaswa'

Makosa mengine ya tahajia/hijai ni kama vile: 'nachukuwa', badala ya 'nachukua', 'jurusa' badala ya 'fursa'.

Alama iliyotuzwa: **11**

## Mtungo wa Nne

**Umepewa dakika 40 kuandika insha yako.**

Andika insha isiyopungua ukurasa mmoja na nusu ukifuata maagizo uliyopewa.

Mwandikie rafiki yako barua ukimshauri kuhusu namna ya kujiandaa vyema kwa mtihani wa KCPE.

SHULE YA MSINGI KINGWEDE,
S.L.P 35,
MSAMBWENI.
9/10/2011.

KWA RAFIKI MPENDWA FATUMA,

Salamu sana au baada ya salamu. Natumai umzima kama kigongo pamoja na aila yako. Je? unaendeleaje katika masomo yako? Nilipata telesi kwamba mamayako alikuwa hali mahututi hoi bin taabani halijui halitambui. Naam, hivyo basi waganga na wanguzi walijaribu kwa miaka na mikaka lakini usaidizi huo uliambulia kidole gumba.

Naam, nia na madhumuni ya kukuandikia waraka huu ni kukushauri kuhusu namna ya kujiandaa vyema kwa mtihani wa K.C.P.E. Nakusii usome kwa bidii kwa udi na uvumba ili uweze kufaulu katika mtihani. usiwe mzembe wala mtundu darasani. Kuwa mkarimu na mpole kwa walimu na hata wanafunzi wenzako kwani wavyele hawakuenda mvange ja soksi ya kiwete walipolonga kwamba mvumilivu hula mbivu.

Ama kweli, ukilima pantosha utavuna pankwisha Nakuomba ulime wakati huu usingoje

wakati wa kiangazi.mahali usipopajua muulize mwalimu wako wa hilo somo na usiogope kuwauliza wakufunzi wako utakuwa wajichimbia 'kaburi' ambalo utaingia mwenyewe na ukumbuke kuwa mficha uchi hazai. Mwisho kabisa nisalimie kitinda mimba wenu na umbusu mara tatu.

Wako mpendwa,

HALIMA HAMADI.

Mtahiniwa huyu ameimudu lugha kiasi. Amezingatia muundo na mtindo wa barua.Ameilewa mada.Hata hivyo, mada haijakuzwa ipasavyo.Insha yake ni fupi mno .Kadhalika ana makosa ya sarufi, hijai na msamiati ambayo yanaupujua muwala wa insha yake.Mifano ya makosa haya ni kama vile::

i) ‘Maututi’ badala ya ‘mahututi’
ii) ‘Wanga na wanguzi’ badala ya ‘waganga na waganguzi’
iii) ‘Mamayake’ badala ya ‘mama yake’.
iv) ‘Mahali’ badala ya ‘suala’/jambo

Alama iliyotuzwa: **20**

### 4.2.4 Kundi la Tatu (Alama 21 – 30)

Insha katika kitengo hiki huwa inaeleweka vizuri. Hudhihirisha kiasi fulani cha ukomavu wa mawazo. Huwa na mshikamano na mtiririko mzuri kiasi wa mawazo. Insha zinazotuzwa alama 21-25 huwa na ubunifu wa kima cha wastani. Aghalabu watahiniwa hupoteza alama kupitia kwa makosa ya sarufi na hijai, matumizi mabaya ya tamathali za usemi na uakifishaji mbaya. Hata hivyo mtahiniwa huwa ameikuza mada vizuri.

Insha zinazotuzwa alama 26-30 huwa na ukomavu zaidi wa mawazo. Maudhui hushughulikiwa kikamilifu zaidi na huwasilishwa kwa mtindo unaovutia zaidi. Insha katika kijitengo hiki hutosheleza urefu. Hata hivyo,insha hizi bado huwa na makosa kiasi ya sarufi na hijai.

## Mtungo wa Tano

**Umepewa dakika 40 kuandika insha yako.**

Andika insha isiyopungua ukurasa mmoja na nusu ukifuata maagizo uliyopewa.

Mwandikie rafiki yako barua ukimshauri kuhusu namna ya kujiandaa vyema kwa mtihani wa KCPE.

Shule ya Msingi ya Dhene.
S.L.P 170
Luanda.
9-11-2011

Habari rafiki mpendwa Elizabeth. Ninatumaini ya kwamba unaendelea vizuri, nasi huku tuko salama. Hakuna ubaya. Baada ya kukusalimia ningependa kukuambia maneno mengine hapa chache tu. Nimejuwa ya kwamba uko katika darasa la nane. Nimejuwa unaenda kufanya mtihani wa K.C.P.E. Ninatumaini kwamba unaenda kupita. usiwe na wasi wasi. Tia tu bidii uombe Mungu atakusaidia. Kuwa na imani kuwa unaenda kupita. Usiogope kwa sababu ni zile mitihani ambayo mnafanya. Tia tu bidii utafaulu. Ita kusaidi maisha ambayo inakuja.

Rafiki wangu nakuambia usiingie katika kikundi ambayo ina weza kukupoteza. Usiogope walimu. Usiposikia kitu darasani ikiwa mwalimu yupo ama hayupo uliza kwani kuuliza si ujinga. Mimi pia tuko katika hiyo msitari. Mimi pia nina enda kuifanya. Na nimejuwa ya kwamba ninaenda kupata.

Usiogope kuja shuleni. Usipokuja, kitu

vitakupitia na ikifanyika hivyo, hiyo unaweza ku-
anguka. Huku nyumbani, kuna wengine ambao wame
tega masikio yao wanataka kusikia kwamba
umepata nini. Itakuwa vibaya ikiwa umefeli
na umetembea miaka nane ikiwa unaenda shuleni.
Kuna wengine ambao wameacha shuleni kama
nawaja maliza ninakuomba usingie katika kikundi
hicho wewe omba tu Mungu ata kusaidia upite
mtihani vizuri. Sisi pia tumejuwa kwamba ako nasi.
Mungu hawachi mja wake

Ukiingia katika nyumba ya mtihani usiogope
fikani tu. Ukiona karatasi usianze kuteteneka. Wacha
woga mlangoni na uingie katika mtihani. Nimejuwa
ya kwamba tutafanya vizuri ikiwa mtihani. Hiyo
ndio maisha yetu tusianezee. Inaweza kutusaidia
baadaye. Kwaheri. Mungu awe nawe katika mtihani

Ni mimi rafiki wako,

Betty Akoth.

Mtahiniwa huyu amedhihirisha kuwa amelielewa na kulimudu swali. Hali ya kuimudu lugha kiasi imebainika pia.Ametumia mtindo na muundo wa barua. Hata hivyo, utungo huu umejaa makosa ya sarufi, msamiati na hijai.Makosa kama vile tafsiri ya moja kwa moja,upatanisho wa kisarufi usiofaa pamoja na uambishaji mbaya yamejitokeza..Ifuatayo ni mifano ya baadhi ya makosa:

i) 'Unaenda kupita' badala ya 'utapita'
ii) 'Uezo' badala ya 'uwezo'
iii) 'Mimi pia tuko katika hiyo msitari' badala ya 'Mimi pia ni katika huo mstari'
iv) 'Usiposikia kitu darasani vitu vitakupita' badala ya 'Usiposikiliza maelezo yatakupita'
v) 'Kikundi ambayo' badala ya Kikundi ambacho
vi) Wameacha shuleni badala ya 'Wameacha shule'
vii) 'Nyumba' ya mtihani badala ya 'chumba' cha mtihani

Alama iliyotuzwa: **24**

**Mtungo wa Sita**

Umepewa dakika 40 kuandika insha yako.

Andika insha isiyopungua ukurasa mmoja na nusu ukifuata maagizo uliyopewa.

Mwandikie rafiki yako barua ukimshauri kuhusu namna ya kujiandaa vyema kwa mtihani wa KCPE.

SHULE YA MSINGI YA WARUKIRA,
S.L.P 19,
KAHETHO.
9-11-2011.

Kwa mpendwa Wanjiru,

Kwanza, ni salamu chekwachekwa kama mchanga wa baharini. Upo? Ninadhani kwamba wewe na wavyele wako mu wazima kama kigongo.

Nachukua fursa hii kukuandikia waraka huu, nikikushauri vile unapaswa kujiandaa vyema kwa mtihani wako wa kitaifa. Bila shaka, Wanjua kuwa MATI ni ngeli ya A-WA. Unapo jiandaa katika mtihani wako unapaswa kufanya mazoezi mengi ipasavyo. Juzi mwalimu wetu wa hesabu alitushauri tunavyoweza kupasi mtihani. Usije ukadhani, mara atakupa alama nyingi kwa unyenyekevu wako. Wanjiru kujitahidi ipasavyo na mwishowe uwe insi anayechumia juani na mwishowe analia kivulini.

Kwanza, asubuhi na mapema, amka alfajiri mbichi kabla kikwala wa pekee kutangaza alfajiri ya mkawini, na ujaribu kufanya majaribio kwa muda wa saa mbili au tatu. Unapofanya mazoezi asubuhi, utakuta kuwa unaelewa zaidi. Kumbuka wahenga na wahenguzi hawakuvalia miwani ya mbao wala soksi za chuma walipong'anda kuwa ukiona vyaelea jua vimeundwa. Hata shuleni unapaswa kuwa mtiifu. Usipokuwa mtiifu mwishowe utakua mti

wronuwa na mazao kamwe. Mathalani ulapogukia patupu kumbuka huwa mwimba wa wijindugu hauambiwi pole.

Naam, pili utakapotia sheria za shule pia waweza kupasi mtihani vizuri. Unapaswa kuwa mtiifu nyumbani, shuleni na popote uendapo. Pia unapaswa kufanya mazoezi si haba. Mtihani unapokaribia, wawezea kununua mitihani na kufanya wewe mwenyewe bila kutegemewa na yeyote. Mfuate mwalimu wako na umuulize maswali yanayokutatiza. Uwe bendera ambayo daima hufuata upepo.

Kila wakati uonapo mtihani, wacha kuwa na wasisi kama mwasi. Kila wasaa lala mapema na uamke mapema kwa kuwa na uzima wa mwili wako. Utakapokuwa ukiyapitia maswali hiyo wakati fanya uchunguzi kutoka kwenye swala hilo. Yawezekana watahini wa mtihani wa kuaifa watauliza swala hiyo mara kadhaa. Kumbuka kuwa mungu hamuachi binadamu wake

Mwisho, uwe mwaminifu ya kwamba utapita ipasavyo. Usiwe na woga mithili ya kunguru ambaye hukimbiza mbawa zake. Itakapofika siku ya kukalia mtihani huo utanishukuru kwa kuwa yatakuwa maswala ambayo umekuwa ukiyapitia. Kama sijaweka kalamu yangu chini nitakuambia kuwa elimu ni funguo za maisha. Uwe na ndoto njema na mafanikio ili uweze kupata maisha mema kama vile 'siku njema huonekana asubuhi. Sina mengi.

Kwaheri.

Wako mwaminifu.

Florence Mukure.

Mtahiniwa huyu ameielewa mada na kuiwasilisha vyema kiasi.Anaimudu lugha kiasi,anajieleza kwa wepesi akilinganishwa na yule wa awali.Mtindo na muundo wa barua umedhihirika.Hata hivyo, utungo huu una athari za lugha ya mama.Athari hii inazua makosa ya hijai na msamiati ambayo yanaufanya mvuto wa insha kudorora.Makosa ya uakifishaji pia yamedhihirika..Baadhi ya makosa ni:

i) 'Kujitahindi' badala ya 'kujitahidi'
ii) 'Kikwala' badala ya 'kikwara'
iii) 'Utakua' badala ya 'utakuwa'
iv) 'Wasisi' badala ya 'wasiwasi'
v) 'Ninadhani' badala ya 'ninatumai'

Alama iliyotuzwa: **26**

### 4.2.5 Kundi la Nne (Alama 31 – 40)

Watahiniwa katika kundi hili kwa kawaida huwa wanaimudu lugha vizuri. Huwa na kiwango cha juu cha ubunifu kimaudhui na kifani. Hutumia lugha kwa wepesi kujieleza. Mijadala/masimulizi yao huwa na muundo bayana wenye mshikamano na mtiririko mzuri wa mawazo. Hawa huielewa mada na kuikuza kwa kiasi cha kuridhisha. Wale wanaotuzwa alama 31-35 huitumia lugha kwa wepesi. Hata hivyo,insha zao huwa na makosa ya hapa na pale ya sarufi, hijai na msamiati.

Wale wanaotuzwa alama 36-40 huwa na umilisi wa lugha wa kiwango cha juu na huwasilisha mawazo yao kwa mitindo mbalimbali ya usimulizi/ mitindo mbalimbali ya kujieleza ambayo huzipa kazi zao mvuto wa hali ya juu. Huteua msamiati unaoafiki mada na kuutumia vyema kufanikisha usimulizi/mjadala wao. Insha zao huwa na makosa machache mno ya sarufi, hijai na msamiati. Hali kadhalika hati zao zinasomeka kwa urahisi na wanatosheleza urefu.

**Mtungo wa Saba**

**Umepewa dakika 40 kuandika insha yako.** BARUA YA KIRAFIKI

Andika insha isiyopungua ukurasa mmoja na nusu ukifuata maagizo uliyopewa.

Mwandikie rafiki yako barua ukimshauri kuhusu namna ya kujiandaa vyema kwa mtihani wa KCPE.

SHULE YA MSINGI YA ILEHO,
S.L.P 666,
KAKAMEGA.
9/11/2011

Kwa rafiki mpendwa Kositi,

pokea salamu nyingi kutoka kwangu. Najua u mzima mithili ya kigongo. Najua unaendelea na kukurukakara za hapa na pale kwa kudurusu vitabu vyako barabara bila uchaka. Usiwe mtu wa kuzurura kama mbwakoko wafanyavyo mitaani. Chambilecho, mgaaga na upwa hali wali mkavu.

Mvuia si mtonjo tafadhali watumie walimu wako vizuri hapo ndipo utafaulu vilivyo. Endelea kuuliza maswali kwa kuwa kuuliza si ujinga wahenga hawakutuacha

bure bilashi. Kumbuka elimu ni ngao ya maisha kwa hivyo fanya bidii kama wafanyakazi mchwa. Ukifaulu wazazi wangu watakuwa na furaha moyoni mwao kama kimnyonyoke aliyetunukiwa shunga la nywele kwa kadamnasi yako. Licha ya hayo utakuwa umepiga kibao mbele kwa wavyele wako kwa kuwa hawangoi wanganga na waganguzi hawakutuvaa soksi za chuma na mikwaju ya mbao punde tu walipo sadiki methali kuwa bidii haiondoi kudura. Kasiti, endelea kuwa kimelea kwa walimu mkijadiliana mambo kadha wa kadha hapo utafaulu masomoni. Punde tu unapokuwa na shida fulani pata msaada kwa walimu wako. Usiwe mwoga kama kunguru kwa kuwa ni mtihani wa kawaida.

Tafadhali kumbuka kuwa heshima si utumwa. Ukitaka kufaulu kuwa mtoto mtiifu, mnyenyekevu, mpole na mwenye hekima. Kumbuka ukikuwa mtoto wa kichwa kigumu basi, utaendelea kufeli mtihani na kuvunga mkia kwelikweli. Mtihani wa kitaifa ndio unaoamua maisha yako ya baadaye. Ukifeli basi mambo yako yataanza kukuendea segemnege na utatiririka machozi kama ngamia. Wazee wa ndemi walio mla mungu hawakutuvisha vilemba vya ukoka walipojilazo kwenye makochi na kusadiki kuwa mtaka cha mvunguni sharti ainame.

Punde tu unapoyazinga tia haya yote utafaulu na kupata alama za juu. Wazazi

wangu wanakuombea na upate alama nyingi
ndipo ~~[illegible]~~ upate wathamini wakukupeleka
katika shule nzuri. Bila shaka nakutakia kila
la heri, Mungu akupe uzima kuja tarehe
ishirini na tisa iwe ni sherehe kuu na
furaha isiyo ya kifani kama ~~[illegible]~~

Mtahiniwa huyu ameilewa mada na kuikuza vyema kiasi. Anajieleza kwa wepesi zaidi akilinganishwa na wale wa vitengo vya chini. Amejipambanua kwa matumizi ya lugh ya kitamathali kama vile sitiari: **Elimu ni nguzo**. Msamiati wake ni mpevu zaidi ukilinganishwa na wa mtahiniwa wa awali. Anatumia msamiati kama vile: **kudurusu** Anaonekana kutumia lugha kwa wepesi na hati yake ni nadhifu yenye kusomeka vyema. Hata hivyo mtahiniwa huyu bado ana makosa ya sarufi, hijai na msamiati. Kwa mfano:

i) **'Mitahani'** badala ya 'mitaani'

ii) **Kulazimisha** msamiati, kwa mfano, 'mwia si mtonjo', 'hawakuvaa soksi za chuma'

iii) Uakifishaji usiofaa

Alama iliyotuzwa: **34**

**Mtungo wa Nane**

**Umepewa dakika 40 kuandika insha yako.**

Andika insha isiyopungua ukurasa mmoja na nusu ukifuata maagizo uliyopewa.

Mwandikie rafiki yako barua ukimshauri kuhusu namna ya kujiandaa vyema kwa mtihani wa KCPE.

TUMBOLILE MAKAO,
SLP 4010,
MBALAMWEZI,
3 Septemba 2011.

Kwa mpendwa Karaha,

Hujambo Karaha? Natumai u buheriwa hamsa wa ishirini. Mimi niko mzima kama ngarange za mvule na wahaka au wasiwasi labda kwako. Natumai unasukuma gurudumu la masomo vyema.

Madhumuni ya kukuandikia barua hii ni kukushauri na kukupa mbinu za kukuandaa vyema kwa mtihani wa kitaifa wa darasa la nane. Kwanza kabisa ningependa kukufahamisha kuwa mtihani huu si mgumu hata kidogo. Mimi niliufanya mtihani huo na nilifua dafu.

Ningependa kukuambia udurusu kwa mapana na marefu. Fanya bidii za duduvule agolaye gogo. Jifunge nira masomoni. Kumbuka ukitaka la waridi sharti udhurike.

Ulienda shuleni peke yako. Wanagenzi hao wengine hawatakuhusu damu wala usaha. Wanagenzi hao wengine wanapopiga soga darasani usiwasikize. Durusu kwa udi na uvumba.

Usiyavalie miwani yale unayoambiwa na walimu wenu. Unapaswa uelewe bayana kuwa asiyesikia la mkuu huvunjika guu. Usiwe sikio la kufa

ambalo halisikii dawa wala kafara. Walimu wako wana tajriba ya kutosha na wanapokuambia kitu wanajua kwa nini. Yazingatie yale walimu tunena darasani.

Uliponiandikia barua mwezi uliopita ulimiambia kwamba unafikiria kukata tamaa. Karatha umemila ng'ombe mzima sembuse mkia. Umekuwa shuleni kutoka darasa la kwanza mpaka darasa la nane. Huu si wakati wa kukata tamaa. Najua katika darasa la nane mambo si rahisi lakini vumilia miezi miwili. Usisahau kuwa mvumilivu hula mbivu aidha baada ya dhiki faraja.

Kile ambacho unafaa kufanya ni kuhakikisha kwamba usome kwa hali na mali. Hakikisha kwamba umesoma kuliko mwanafunzi yeyote nchini. Andika kwenye daftari lile ambalo umesoma bila kuangalia mahali halafu urudi kwenye kitabu kulinganisha. Najua wewe si wembe butu masomoni. Usiwe na wahaka wa kuku mgeni.

Pia ukiwa na swali uliza. Kuuliza si ujinga. Wacha wale wanafunzi wengine waseme wanachotaka. Maneno hayo unafaa uyapuuze. Hayafai kufanya upandwe na mori.

Unafaa pia kupiga bismilahi kila siku. Kaski moja haifai kupita kabla hujapiga dua na kwa sababu Mungu si adhumini aidha Mungu si mtovu utopasi katika mtihani wako wa

kitaifa. Usife moyo. Yazingatie liayo na ukumbuke kufanya bidii za mchwa ajengaye kichuguu kwa mate.

Mimi wako wa juu na mvua,
Tumbolile Makao.

Mtahiniwa huyu amedhihirisha ubunifu zaidi akilinganishwa na yule wa awali. Badala ya kutoa ushauri kana kwamba yeye pia anaufanya mtihani, anabainisha kwamba aliufanya mtihani wa aina hii mwaka uliopita,hivyo anajitoa kama mfano wa waliopitia hali hii na kufaulu..Kadhalika, anahusisha tukio hili la kuandika barua na tukio la awali. Mwenzake amemwandikia barua ,naye anaijibu.Hali hii inaupa utungo wake shani na mvuto zaidi. Kadhalika, lugha yake ni pevu zaidi ikilinganishwa na insha za kitengo cha chini.Uteuzi wake wa lugha na tamathali za usemi unaafiki nasaha anayotoa.Makosa ya sarufi na hijai ni machache mno.Mfano wa makosa haya ni:**Adhumani** badala ya **Athumani.**

Alama iliyotuzwa: **37**

## 4.3 MAPENDEKEZO KWA WALIMU

4.3.1 Walimu wawahimize wanafunzi kufanya mazoezi zaidi katika mada tata za sarufi.

4.3.2 Ufunzaji wa msamiati uhusishwe na muktadha badala ya kuufunza ukiwa mkavu. Kwa mfano msamiati wa magonjwa unaweza kufunzwa kwa kutumia ufahamu kuhusu magonjwa.Hili litamwezesha mwanafunzi kuuelewa msamiati katika matumizi halisi.

4.3.3 Wanafunzi wahimizwe kutumia ujuzi wa waliyosoma katika ufahamu kujibu maswali ya ufahamu badala ya kukariri/kuchopoa mawazo moja kwa moja kutoka kwenye vifungu.

4.3.4 Wanafunzi wahimizwe kutumia mbinu bora za kuukabili ufahamu. Badala ya kusoma swali, kisha kuanza kutafuta majibu, wasome ufahamu kwanza kabla ya kuyasoma maswali na majibu yaliyotolewa.

4.3.5 Walimu watunge maswali yanayopima stadi mbalimbali(ngazi/viwango tofautitofauti vya maarifa au utambuzi wala si stadi ya kukariri/ujuzi pekee. Hili litamzoesha mwanafunzi kujibu maswali ya aina tofautitofauti katika mtihani.

4.3.6 Stadi ya kusikiliza na kuzungumza ihimizwe zaidi kupitia utambaji, mijadala na imla, ili kuboresha maendelezo na kuimarisha mitindo ya kujieleza/mitindo ya usimulizi..

4.3.7 Wanafunzi wasisitiziwe umuhimu wa kusoma vitabu na makala mbalimbali ili kukuza ubunifu.

4.3.8 Wanafunzi waonywe dhidi ya kushinikiza msamiati usiohitajika katika insha. Hili hufifilisha mawasiliano na kuifisidi insha mvuto wake.Msamiati unaoteuliwa sharti uoane na mada na kuafikiana na msamiati/matini jirani katika sentensi ambamo umetumiwa.Msamiati wa kishairi usitumiwe kuandika tungo zisizo za kishairi.

4.3.9 Walimu warejelee vitabu mbalimbali vilivyopendekezwa, wasitumie kimoja tu. Hili litawapa wanafunzi uwanja mpana wa kujifunzia.

4.3.10 Walimu wawasisitizie wanafunzi umuhimu wa hati nzuri ili kurahisisha usomaji na usahihishaji wa insha zao na kuzipa kazi zao mvuto chanya.

4.3.11 Walimu wawahimize wanafunzi kutumia Kiswahili zaidi katika mazungumzo yao ili kuimarisha mikakati ya kujieleza na kusimulia kwacho.

4.3.12 Walimu wawaelekeze wanafunzi kuhusu namna ya kufasiri mada/maswali mbalimbali ili kukinga dhidi ya kupotoka kimaudhui.

4.3.13 Walimu wawape wanafunzi mazoezi ya mitindo tofautitofauti ya insha ili wapate uzoefu wa kuandika aina mbalimbali za insha.

4.3.14 Walimu watumie mwelekeo mseto katika ufunzaji wa mada mbalimbali, kwa mfano mada changamano za kisarufi..Mathalan, mwalimu anaweza kutumia vitabu vya hadithi kufunzia dhana za kisarufi kama vile njeo,hali na aina za maneno. Hili litakinga dhidi ya wanafunzi kuziona dhana hizi kuwa dhahania. Itakuwa rahisi kuzielewa dhana hizi zikitokea katika matumizi halisi. Kadhalika hili litayafanya mafunzo ya sarufi kuwa ya kuvutia zaidi, hivyo wanafunzi watayachangamkia na kuyaelewa zaidi.